# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## MKUTANO WA NANE

## YATOKANAYO NA KIKAO CHA NNE

**8 SEPTEMBA, 2017**

## MKUTANO WA NANE

## KIKAO CHA TATU TAREHE 8 SEPTEMBA, 2017

### I. DUA:

Saa 3:00 asubuhi Mhe. Job Yustino Ndugai (Spika) alisoma Dua na kuongoza Kikao cha Bunge.

Makatibu Mezani:

1. Ndg. Ramadhani Issa Abdallah
2. Ndg. Laurance R. Makigi

### II. TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Job Y. Ndugai (Mb) Spika alitoa Taarifa kuhusu Tukio la kushambuliwa kwa Mhe. Tundu Antiphas Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki (CHADEMA). Spika alieleza jinsi tukio lilivyotokea, matibabu katika Hospitali ya Mkoa wa Dodoma na kusafirishwa kwa Mhe. Tundu Antiphas Lissu kwenda Hospitali ya Agha Khan nchini Kenya na sababu za kupelekwa huko.

Aidha, Mhe. Spika alielezea juhudi za kuwatafuta wahalifu, umuhimu wa kuwepo kwa utulivu nchini kutokana na tukio hilo ambalo ni la kipekee kutokea kwa Mbunge kupigwa risasi wakati Bunge likiwa kazini na pia aliwaomba Wabunge kujitolea kuchangia nusu ya posho kwa siku kumsaidia gharama za matibabu Mhe. Tundu Antiphas Lissu.

### III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano aliwasilisha Mezani Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki Nyongeza ya Tano ya Mwaka 1994, Itifaki Nyongeza ya Sita ya Mwaka 1999, Itifaki ya Nyongeza ya Saba ya Mwaka 2004, Itifaki Nyongeza ya Nane ya Mwaka 2008 na Nyongeza ya Tisa ya Mwaka 2016 ya Katiba ya Umoja wa Posta Duniani.

Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, aliweka Mezani Maoni ya Kamati ya Miundombinu juu ya Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki Nyongeza ya Tano ya Mwaka 1994, Itifaki Nyongeza ya Sita ya Mwaka 1999, Itifaki ya Nyongeza ya Saba ya Mwaka 2004, Itifaki Nyongeza ya Nane ya Mwaka 2008 na Nyongeza ya Tisa ya Mwaka 2016 ya Katiba ya Umoja wa Posta Duniani.

Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano aliwasilisha Mezani Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki Nyongeza ya Tano ya Mwaka 1994, Itifaki Nyongeza ya Sita ya Mwaka 1999, Itifaki ya Nyongeza ya Saba ya Mwaka 2004, Itifaki Nyongeza ya Nane ya Mwaka 2008 na Nyongeza ya Tisa ya Mwaka 2016 ya Katiba ya Umoja wa Posta Duniani.

## IV. MASWALI:

Maswali yafuatayo yaliulizwa na kujibiwa kama ifuatavyo:-

### OFISI YA WAZIRI MKUU

Swali Na. 39: Mhe. Joseph George Kakunda

Nyongeza: Mhe. Joseph George Kakunda

### WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI

Swali Na. 40: Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka

Swali Na. 41: Mhe. Rashid Abdallah Shangazi

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Swali Na. 42: Mhe. Martin Mtonda Msuha

Nyongeza: Mhe. Amina Saleh Mollel

Swali Na. 43: Mhe. Venance Methusalah Mwamoto

Nyongeza: Mhe. Flatei Gregory Massay
Mhe. Anna Joram Gidarya

**WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

Swali Na. 44: Mhe. Willy Qulwi Qambalo
Nyongeza: Mhe. Willy Qulwi Qambalo

Swali Na. 45: Mhe. Oran Manase Njeza

Nyongeza: Mhe. Ally Mohamed Kessy

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

Swali Na. 46: Mhe. Faida Mohammed Bakar

Swali Na. 47: Mhe. Zubeda Hasani Sakuru

**WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Swali Na. 48: Mhe. Kapt. (Mst) George Huruma Mkuchika

Nyongeza: Mhe. Nape Mosses Nnauye

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Swali Na. 49: Mhe. Azza Hillal Hamad

Nyongeza: Mhe. Azza Hillal Hamad

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Swali Na. 50: Mhe. Maftaha Abdallah Nachuma

Nyongeza: Mhe. Maftaha Abdallah Nachuma

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Swali Na. 51: Litapangiwa siku nyingine

## VI. MATANGAZO:

Mhe. Spika aliwatambulisha Wabunge wageni mbalimbali waliohudhuria Bunge ikiwa ni pamoja na wageni waliokuja kujifunza Shughuli za Bunge.

## VII. MWONGOZO WA SPIKA:

Baada ya kumalizika kwa Matangazo Mhe. Spika alipokea Miongozo kutoka kwa Wabunge wanne kama ifuatavyo:-

(i) Mhe. Hussein Mohamed Bashe kwa kutumia Kanuni 47(1 na 2) aliomba jambo la dharura. Mhe. Hussein Mohamed Bashe aliomba Mwongozo kwa kujadili matukio ya usalama kwa Wabunge na Wananchi kwa ujumla hapa nchini. Hasa kutokana na Mbunge Tundu Antiphas Lissu kupigwa risasi jana tarehe 7 Septemba, 2017 nyumbani kwake mchana saa 7:00 hivyo aliomba suala hili lijadiliwe na Kamati ya Mambo ya Nje, Usalama na Ulinzi kwa kuwaita wadau mbalimbali wa masuala ya usalama.

Katika hili Mhe. Spika alitoa Mwongozo kwamba amekubaliana na Mwongozo wa Mhe. Hussein Mohamed Bashe na kulipeleka suala hili kwenye Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na suala hili lianze moja kwa moja na Taarifa kuwasilishwa Bungeni kabla ya Bunge kumalizika.

(ii) Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara naye alimuunga mkono Mhe. Hussein Mohamed Bashe kwani alikuwa na hoja hiyo hiyo.

(iii) Mhe. Joshua Samweli Nassari naye Hoja yake ilikuwa inafanana na Hoja ya Mhe. Hussein Mohamed Bashe.

(iv) Mhe. Goodluck Araph Mlinga alitoa Hoja kwa mujibu wa Kanuni 68(7) kuhusu majibu yasiyoridhisha ya Serikali, alitoa mfano kuna Mawaziri wanatoa ahadi ya kutembelea Majimboni wakati ukifika hawaendi Majimboni, nini kifanyike kuwadhibiti Mawaziri wanaoshindwa kutimiza ahadi zao. Katika hili Mhe. Spika alitoa Mwongozo kwamba, kama ikitokea hivyo Mbunge anaweza kumwandikia Spika na atatafutiwa ufumbuzi.

**(v) HOJA ZA SERIKALI:**

**MAAZIMIO:**

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:

Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki Nyongeza ya Tano ya Mwaka 1994, Itifaki Nyongeza ya Sita ya Mwaka 1999, Itifaki ya Nyongeza ya Saba ya Mwaka 2004, Itifaki Nyongeza ya Nane ya Mwaka 2008 na Nyongeza ya Tisa ya Mwaka 2016 ya Katiba ya Umoja wa Posta Duniani.

Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa, Waziri wa Ujenzi na Mawasiliano na Uchukuzi aliwasilisha Hoja yake kuhusu Azimio hilo.

Mhe. Moshi Selemani Kakoso alliwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Azimio lililowasilishwa hapo juu.

Mhe. Willy Qulwi Qambalo aliwasilisha Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio lililowasilishwa hapo juu.

Katika Hoja hii hakuna Wabunge waliochangia Hoja ndipo Mhe. Naibu Spika alimwita Mtoa Hoja kuhitimisha Hoja yake.

Mhe. Naibu Spika alihoji Bunge kuhusu Azimio lililowasilishwa na Hoja ilikubaliwa na Bunge.

## (vi) KUAHIRISHA BUNGE

Saa 5:57 Mchana Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu saa 3:00 asubuhi.